# *Uwekezaji*

Asante sana. Karibu ningependa kueleza hisia zangu, kama Ndugu Palmer alivyosema, "Mimi ni msikilizaji mzuri." Hakika nilifurahia jambo hili, asubuhi ya leo, nisingalikosa huku kuwasikia hawa ndugu mbalimbali hata iweje, na wale wanaotoa shuhuda hizi.

2 Yule ndugu ambaye ameimba hivi punde amekuwa akija kanisani mwetu kule juu, na nanii wake. . .Nimemjua mama yake na dada zake, hapa, kwa, loo, kwa miaka mingi. Sijawahi kufika maskanini kwa wakati mzuri kumsikia akiimba, na nilikuwa nikitaka tu kulipendekeza, ndipo nikaja, ikasemekana atauimba. Ndugu, hapa, alisema a—angeuimba pia, kwa hiyo nikasema, "Unaweza kuimba wako usiku wa leo." Kwa hivyo, tutafurahi kuusikia huo.

3 Daima ni ma. . .majaliwa makuu sana kuwa huku, ambako, Uwepo wa Bwana. Huku kukiweko, kama ndugu yetu alivyosema, kwamba kuna umwili mwingi sana katika madhehebu yetu mbalimbali unaotutenganisha, na, lakini kunao Mwili, Mwili wa kisiri wa Kristo, Huo ndio Mwili ambao sote tunaingia kwa Roho mmoja, tukabatizwa kuwa Mwili huo mmoja, ndipo tunakuwa raia wa Ufalme wa Mbinguni.

4 Sasa, ninaamini ya kwamba tunapaswa kuwa tumetoka hapa saa si-. . .[Mtu fulani anaongea na Ndugu Branham—Mh.] (Ati nini?) ["Tunaweza kuondoka baada ya saa sita."] Loo, je, huo tu ndio muda nilio nao, saa mbili pekee? Kidogo nimevunjika moyo. Mnajua, inanichukua muda mrefu kusema kile ninachowazia, lakini, nashukuru kwa ajili ya kusanyiko linalonivumilia, lakini nilikuwa tu nikisema hivyo. Sasa, maneno machache tu kwa wafanyabiashara na wote walio hapa.

5 Nami ninataka kusema umekuwa ni wakati mzuri; jana jioni moyo wangu ulichangamka, hata nilipofika nyumbani, kama walivyosema, John Wesley alivyosema, kuhusu "kifuani mwake," kuona kwamba Mungu wetu angali hai. Wala haitubidi kudhania juu ya hili, Yeye ni—Yeye ni halisi, ni ule urahisi wa kukubali tu yale ambayo amesema na kuyaona yakifanywa halisi, mnaona, Neno ni Mbegu, na kama Mbegu hiyo ikiwekwa katika udongo mzuri chini ya halijoto ifaayo, itakua endapo imerutubishwa, nasi tunajua Neno hili limerutubishwa, kwa sababu ni Mungu Mwenyewe, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," Angali ni Mungu, "Alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu."

6 Tunashukuru sana kuwasikia Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri, Mwothodoksi wa Kiyunani, na wote pamoja,

wakija pamoja katika sehemu moja kuu. Nami naamini Yakobo alichimba kisima, ndipo adui akamfukuza, naye akakiita "Uovu," akachimba kisima kingine, nao walikuwa wamemfukuza, na kukiita "Ugomvi," akachimba kisima kingine, na kusema, "Kuna nafasi kwa ajili yetu sote." Kwa hiyo, nafikiri hivyo karibu ndivyo ilivyo, Luther alichimba kimoja, naye Wesley akachimba kimoja, sasa tuna kimoja, kuna nafasi kwa ajili yetu sote. Kwa hiyo, na tusimame tu sote na kukinywea kisima hiki kimoja. Endapo unampanda ngamia mwenye nundu moja, au ngamia mwenye nundu mbili, au ngamia mwenye nundu tatu, bado unaweza kuja na kunywa, hayo tu, tuko safarini mwetu.

7 Nafikiri sasa, baada ya hisia zetu ndogo za ucheshi na kadhalika, kwa kuwa nafikiri ni mzuri, hata Mungu Mwenyewe ana ucheshi, mwajua, nafikiri inatupasa tu kuinamisha vichwa vyetu kwa muda, kabla ya kulikaribia Neno hili, kwa maombi.

8 Baba yetu, Mungu mkuu na mwenye enzi, Ambaye, mwimbaji wetu ameelezea hisia zetu zote, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu," tunakukaribia Wewe katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Bwana Yesu, Dhabihu yetu, na tunapokuja kutoka kwenye jengo hili kuingia katika Uwepo Wako kwa imani, tunaangalia huko kwenye Dhabihu yetu kwenye Kiti Chako cha Enzi, tukijua ya kwamba ametuahidi tukiomba lolote kwa Jina Lake tutapewa. Tutajaribu kusoma Neno Lako na kulizungumzia. Sasa, jalia Roho Mtakatifu alichukue Neno na kulipanda ndani ya mioyo ya kila mmoja wetu, itahiri midomo inenayo na masikio yasikiayo, pia jalia lianguke kwenye udongo mzuri na kuzaa mara mia moja. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

9 Kama...Watu wengi hupenda kuchukua mahali katika Maandiko, kwa kawaida, wanaposoma wahudumu, ningependa kuvutia usikivu wenu kwenye Injili ya Marko Mtakatifu mlango wa 10, kuanzia kifungu cha 17, kwa ajili ya somo tutoe kwenye muktadha huu:

> *Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja* akamjia *mbio,* akampigia magoti, *akamwuliza, Mwalimu Mwema, nifanye...ni—nipate kuurithi uzima wa milele?*
>
> *Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu.*
>
> *Wazijua amri, Usizini, Usiue, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu* na...*Waheshimu baba na mama yako.*
>
> *Akajibu akamwambia, Mwalimu,* mambo *hayo yote nimeyashika tangu utoto wangu.*
>
> *Yesu akamkazia macho,* akampenda, *akamwambia, Umepungukiwa na neno moja: enenda, ukauze ulivyo*

navyo *vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni: kisha njoo ujitwike msalaba* wako, *unifuate.*

*Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni: kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*

10 Ningependa kutoa so—somo kutoka hili juu ya somo la *Uwekezaji.* Nami nilifikiri huenda hili likafaa kwa dakika chache, kuwazungumzia wafanyabiashara wa hili jiji juu ya uwekezaji, kwa sababu kwamba mfanyabiashara yeyote daima, iwapo ni mfanyabiashara mzuri, huvutiwa na uwekezaji mzuri. Hilo linaonekana kuwa ndilo wanalopenda kufanya, ni kufanya uwekezaji m—mzuri, uwekezaji thabiti, kwa sababu unaleta faida, kila wakati.

11 Basi asubuhi ya leo nataka kuzungumza nanyi watu, kama, kama kuna wengine hapa, ninii...juu ya uwekezaji bora sana niujuao. Wakati fulani uliopita niliulizwa swali na mhudumu mashuhuri wa kanisa la Baptisti, ambamo nilitoka, akasema, "Ndugu Branham, nasikia ya kwamba uko pamoja na Wafanyabiashara wa Full Gospel."

Nikasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli."

Akasema, "Je, una shughuli gani na Wafanyabiashara wa Full Gospel?"

Nikasema, "Mimi—mimi ni mfanyabiashara."

Akasema, "Mfanyabiashara?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Kasema, "Kwani unafanya biashara gani?"

Nikasema, "Bima." [Eng. "Insurance."—Mfa.]

Naye akasema, "Ati nini?"

Nami nikasema, "Dhamana." [Eng. "Assurance."—Mfa.]

Kasema, "Ya aina gani?"

Nikasema, "Uzima wa Milele."

Endapo yeyote, ninyi jamaa mnataka kuzungumzia hati ya mkataba pamoja nami, baada ya mkutano, nitafurahi kukutana nanyi, na—na kuizungumzia.

12 Wakati fulani uliopita, rafiki ambaye nilisoma naye shuleni, yeye ni wakala wa bima, na ni mtu mzuri, ninaye ndugu ambaye ni wakala wa bima, lakini ilitokea tu kwamba sikuwahi kuwa na bima, na kwa hiyo mimi, sina neno dhidi yake, lakini mimi... huyo mvulana alikuja wakati mmoja, jina lake ni Snyder, ndugu yake ni mhudumu wa Kibaptisti, Wilmer akaniambia, akasema, "Billy, ningependa kuzungumza nawe kuhusu bima fulani."

Nami nikasema, "Wilmer, asante," Nikasema, "Ni—nitazungumza juu ya kitu kingine chochote, lakini," nikasema, "ninayo bima tayari."

Naye akasema, "Loo, samahani." Akasema, "Ati una nini?"

Nikasema, "Nina dhamana."

Naye. . .Ndipo mke wangu akaniangalia kana kwamba nilikuwa ni mwongo, akasimama, naye akanikazia macho, maana sina bima yoyote.

Naye akasema, "Billy, una bima gani?"

Nikasema, "Nilisema, 'Dhamana.'"

> Dhamana iliyobarikiwa, Yesu ni wangu!
> Loo, ni kionjo cha kimbele kilioje cha utukufu wa Kiungu!
> Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na Mungu,
> Nimezaliwa kwa Roho Wake, nikaoshwa katika Damu Yake.

Akasema, "Hiyo ni nzuri sana, Billy, lakini haitakuweka hapa makaburini."

13 Nikasema, "Itanitoa, sina wasiwasi kuhusu kuingia, nataka kutoka." Kwa hiyo, sijisumbui juu ya kuingia mle, ni kutoka. Kwa hiyo, hilo ndilo ninalotaka kuzungumzia.

14 Jamaa aliye na pesa anataka kuziweka kwenye uwekezaji mzuri, bila shaka. Mtu ambaye, ana kadiri, tuseme, ya dola elfu kumi, angependa kuziweka kwenye uwekezaji fulani. Usiziweke mfukoni mwako, maana unajua wezi wataziiba, na kwa hiyo, hutaki kufanya hivyo. Kwa hiyo, unataka, ikiwa wewe ni mfanyabiashara mzuri, stadi, unataka kuziweka kwenye kitu ambacho kitaninii. . .kitaleta faida, unataka kuzikopesha kwa riba, unajua kuhusu zile talanta katika Biblia, kwa hivyo inakubidi kuziweka kwenye matumizi fulani ambayo yataleta faida, biashara nzuri, imara.

15 Halafu basi, kwa kufanya hivi, hutaki kuziweka katika kitu fulani kisicho imara, hakuna mtu ambaye angetaka kufanya hivyo. Mfanyabiashara mzuri na stadi hangefikiria kitu kama hicho, ninyi watu msingefanya hivyo, kuziweka katika kitu ambacho, mojawapo wa huu hapa, utajiri wa lala maskini amka tajiri wala hujui unatoka wapi, afadhali uwe mwangalifu kuhusu hilo, utapoteza yote uliyo nayo, maana ni bahati nasibu. Nayo bahati nasibu si biashara nzuri, imara, ni. . .ina kubahatisha, wala, hutaki kujaribu bahati za aina hiyo, lakini unataka kuziweka katika kitu fulani, katika kampuni fulani nzuri, imara, inayoleta faida kubwa, kitu ambacho ni thabiti, cha kutegemewa, kitu ambacho unajua kwamba kimeleta faida, na kimethibitika kwamba kina faida. Unapokuwa na kitu kama hicho cha ku-. . .kuwekezea, mbona, basi unajisikia kuhakikishiwa kwamba u—utapata kitu, unaweza kujua yakini unapoweka pesa zako hapo, lakini ikiwa biashara si nzuri sana, vema, usingetaka kujaribu hiyo, mpango mzuri, unaoaminika, kitu ambacho kingekuletea faida nzuri.

16 Basi huyu mtawala kijana tajiri, kama tunavyomwita katika Biblia, aliacha nafasi nzuri sana, alikuwa na nafasi ya kuweka utajiri wake wa dunia hii katika mpango uliohakikishwa, lakini alishindwa, hakufanya hivyo. Alipewa nafasi ambayo angeweza kupata riba kwake, na kufanya uwekezaji mkubwa, lakini a—akashindwa kuikubali fursa hiyo, sana, kama wengi wetu wafanyavyo siku hizi, nasi tunaona kwamba ni vibaya sana, lakini tunalifanya, sasa, ingawa mpango huu ambao alipewa ulithibitishwa kikamilifu kwamba ulikuwa ni mzuri. Yesu alipokuja duniani, alithibitisha kwamba alikuwa kile alichosema alikuwa, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, kwa maana aliuleta kwenye shi—shindano la kuamua na kusema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi."

17 Kwa hiyo, huyu kijana mwanamume alikuwa kama wakati huu wa Laodikia mkuu na tajiri tunamoishi, waliona nafasi kubwa ku—kuwekeza katika kitu fulani, lakini hakipendwi sana. Yesu hakuwa Mtu maarufu katika siku Zake, ila tu miongoni mwa maskini na wasio na elimu, kanisa la siku Zake, madhehebu ya siku Zake, au, dini za kimadhehebu, hazikuwa na uhusiano wowote Naye, lakini hapana shaka kulikuwa na jambo *fulani* kumhusu, ambalo huyu kijana mwanamume tajiri aliona ndani ya Yesu, ambalo hakuliona kwa wengine. Na kweli alikuwa na akili timamu, nzuri ya kuja na kuuliza afanye nini, kwa sababu alikuwa ameona katika Yesu kwamba kulikuwa na sifa ambazo ninii yake. . .hakuiona kwa mtu mwingine yeyote, lakini, mnaona, alikuwa tajiri sana kwa mambo ya ulimwengu. Tunayo picha nzuri ya jambo hili katika Wakati wa Laodikia katika Ufunuo 3, "Kwa sababu wasema wewe ni tajiri wala huna haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa u mnyonge, maskini, kipofu, mwenye mashaka, uchi, wala hujui."

18 Hilo ni wazo la kutisha jinsi gani, kuwazia ya kwamba mtu angeweza kuwa kipofu, au angekuwa uchi barabarani, hilo ni jambo la kutisha, lakini sehemu yake mbaya zaidi ni, ni mtu aliye katika hali hiyo, naye hata hivyo hajui. Ikiwa mtu huyo angejua kuwa yuko katika hali hiyo, angejaribu kujisaidia, lakini akiwa katika hali hiyo naye hajui yuko katika hali hiyo, wala huwezi kumwambia lolote tofauti.

19 Hiyo ndiyo picha tunayoiona siku hizi, ya kwamba, wengi wetu watu tunamwona Mungu akitenda kazi katika siku hizi za mwisho, tunamwona Roho Mtakatifu akija miongoni mwetu, na kuthibitisha ahadi zile zile za Biblia ambazo Kristo alisema zingetukia, na hata hivyo, pamoja na tofauti zetu za kimadhehebu, na kanuni zetu za imani, na hadhi zetu za kijamii, kama yule kijana alivyokuwa nayo, tunaikataa hiyo nafasi kama anavyofanya yeye, ama, kama alivyofanya. Waliogopa kuwekeza, afadhali ashikilie vitu alivyokuwa navyo: umaarufu, pesa, tamaa, badala ya kuwekeza, wakati yeye. . .nafasi ilipobisha

mlangoni pake, kwa Ufalme wa Mungu.

20 Siamini kwamba mtu yeyote, ambaye. . .anayempenda Kristo, angeweza kuketi katika mkutano, kama inavyotukia katika mmiminiko halisi wa Kipentekoste, uliojazwa na Roho katika siku hii, na kuona Uwepo wenyewe wa Yesu Kristo ukiwashukia watu, na kutenda, na kufanya mambo ambayo Yeye aliahidi yangefanywa katika siku hii, na (njia pekee unayoweza ni. . .) kuikataa hiyo nafasi ambayo Mungu amekupa ya kuwa sehemu yake.

21 Ni jambo la kijinga jinsi gani alilofanya kijana mwanamume huyu, kuikataa nafasi hii, nayo madhehebu yanafanya jambo la kijinga jinsi gani siku hizi, badala ya kumkubali, na kumkumbatia Roho Mtakatifu, na kusahau tofauti zao, wanatenganisha udugu na kujaribu kuvuta vikundi vidogo kuwafuata wao.

22 Tunaona, ya kwamba katika Ufunuo 3, kwenye Wakati wa Laodikia, ambao tunaishi ndani yake sasa, kwa tafsiri yangu ya Maandiko, ya kwamba wakati Ujumbe umetolewa wa Wakati wa Laodikia, kama ulivyofanya katika kila wakati, na kila wakati ulikuwa na mjumbe, kwamba tunakuja katika siku hizi za mwisho, na kuona ya kwamba kanisa hilo lilikuwa tajiri sana, nao hawakukubaliana na Yeye kabisa, wakamwondosha kanisani, kwa sababu ndio wakati pekee wa kanisa tunaoona, hata kupitia, vema, tungewazia Wakati wa Kanisa la Efeso, na Sardi, na nyakati zote za kanisa jinsi zilivyokuwa, hata kufikia Wakati wa Filadelfia, loo, Wakati wa Kanisa la Wesley, na kadhalika, hata katika nyakati hizo zote, hakutupwa nje, bali katika Wakati wa Kanisa la Laodikia Yeye alikuwa nje, lakini alikuwa angali anabisha, akijaribu kuingia katika kanisa Lake Mwenyewe.

23 Pamoja na Uwepo Wake wa Kiungu, kama ilivyokuwa alipokuwa duniani, Mungu alikuwa katika Mtu mmoja, sasa Mungu yuko ndani ya Kanisa Lake, Uhai Wake umegawanyika miongoni mwa watu Wake, Mungu akiishi miongoni mwao, akijaribu kuwaunganisha pamoja katika Mwili wa siri wa Kristo, unaoitwa Bibi-arusi Wake. Na wakati anapojaribu kufanya hivyo. . .Naye atafanya hivyo, kwa maana kama nabii alivyosema, ilitokea, mtangulizi Wake wa Kuja Kwake Mara ya Kwanza, alisema, "Mungu anaweza katika mawe haya kuwainua watoto." Na siku hizi, wakati baraka zilipowashukia Wapentekoste miaka mingi iliyopita, nao wakajitenga, wakionekana kama hawana imani, Mungu anaweza kutoka kwa Methodisti, na Orthodoksi, na kadhalika, katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.

24 Basi mliwahi kuwazia, ndugu zangu, mliwahi, iliwahi kuwajia katika Maandiko, ya kwamba siku ile ile ambayo bikira aliyelala alikuja kununua Mafuta, hiyo ndiyo

siku aliyokuja Yeye? Unapoona Orthodoksi ya Kiyunani, Waepiskopali, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, wakiingia, wakimwonea Huyu njaa, "Tunaweza kupata wapi mafuta haya," kumbuka, saa hiyo ndiyo aliyokuja Bwana arusi. Hebu tuangalie uwekezaji wetu, ambapo unaletea faida.

25 Sasa, walimwondosha madhehebuni mwao, hawakumtaka. Yule mtawala kijana tajiri alienda zake mwenye huzuni, ingawa mnaona ya kwamba inasema hapa katika Maandiko, "Yesu alipomkazia macho alimpenda." Naye amewapenda watu hawa katika mashirika haya, wao ni watu wa Mungu, aliwapenda, na ametoa, na ametoa kwa miaka hamsini iliyopita, nafasi ya kufanya uwekezaji mwingine ndani Yake, sio katika mjengo wa kanisa, bali katika uwezo na ufufuo wa Kristo, na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sio maarufu, bila shaka sio, haujawahi kuwa maarufu. Chochote ambacho Mungu aliwahi kutenda duniani hakikuwa maarufu tangu mwanzo, kinachukiwa sana, imekusudiwa kuwa hivyo. Je, Yesu hakuwaita Mafarisayo kuta zilizopakwa chokaa? Kasema, "Ni yupi kati ya baba zenu ambaye hakuwatesa manabii? Mnayapaka makaburi yao chokaa, lakini ninyi ndio mliowaweka humo ndani."

26 Wanayajenga juu ya kitu kikubwa mno, Mmethodisti juu ya John Wesley, mtu mashuhuri, Lutheri juu ya Martin Luther, na kadhalika, na sasa, Wapentekoste wanajaribu kujengea kitu fulani kaburi, kilichokuwako miaka hamsini iliyopita, kilichowatoa katika machafuko ya aina hiyo, na sasa, wanakirudisha moja kwa moja ndani tena, waking'arisha ka—kaburi la wale ambao kwa kweli tuliweka mle ndani. Hiyo ni kweli.

27 Sasa, hati hii kuu ya dhamana ambayo ninamwomba kila mmoja kuwekeza ndani yake leo hii, hebu tuangalie nyuma, na mambo yote yanapaswa kuwa kama shughuli zingine zozote, kabla hatujawekeza, tunapaswa kutafuta kujua mambo ya kuhusu—kuhusu hiyo kampuni, au kuhusu kitu ambacho tunajaribu kununua. Nami nafikiri lingekuwa ni jambo jema, asubuhi ya leo, katika dakika hizi chache zijazo, kama tungechunguza baadhi ya wenye hati hizi tuone mambo yaliendaje hasa, hiyo ndiyo njia pekee ya kufanya unapoenda kuwekeza kibiashara. Kwa kawaida utamwendea na kumwambia mtu mwenzako, "Ninii . . . Vipi kuhusu kampuni *fulani-na-fulani* hii? Vipi kuhusu biashara *fulani-na-fulani* hii?"

28 "Vema, ilimfanyia *hivi Fulani-wa-fulani*. Ilimfanyia *hivi Fulani-wa-fulani*, na vema, ilileta faida kwenye *hii*. Nazo dhamana hizi, kuponi hizi, kuponi za benki ya serikali, nazo zilileta faida ya asilimia ishirini na tano," na kadhalika.

29 Hiyo . . . Ni vizuri kuchunguza, upate kujua kabla ya kuweka.

30 Kwa hivyo, kama ninii. . . si hasa wakala wa dhamana asubuhi ya leo, lakini ninazungumza kwa niaba ya Mmoja, hebu turudi nyuma na kuchunguza, tupate baadhi ya walio nayo, baadhi ya waliokuwa na kile Kitu ambacho nimekuwa nikijaribu kuwaambia mshikilie, hicho ni Neno la Mungu, Neno la ahadi Yake bila kujali madhehebu au kanuni za imani, wanaume na wanawake ambao waliliamini Neno la Mungu, bila kujali mtu mwingine yeyote aliwazia nini juu yake, tunataka kuwatafuta baadhi ya waliokuwa nazo na kuwachunguza.

31 Hebu tuanze kule nyuma na m—mzee aliyekuwa nayo, ambaye ningeweza kumwazia, miaka mingi iliyopita. Jina lake lilikuwa Nuhu, alikuwa mkulima tajiri, nasi tunaona ya kwamba alipokuwa na mali nzuri juu ya nchi, siku moja Mungu alizungumza naye, na kwa kawaida Mungu anapozungumza, ni kinyume sana na mawazo ya kilimwengu ya jambo hilo, ni tofauti sana na mtindo wa kisasa, mpaka mtu anayepokea hati hiyo ya mkataba, hao watu wengine ambao hawana hati ya mkataba, wala kujua lolote kuihusu, hawajawahi kuizungumzia, wanafikiri huyo mtu ana kichaa kwa kuikubali, sikuzote imekuwa hivyo.

32 Mungu alimwambia Nuhu, kwa ahadi, "Ninaenda kuangamiza ulimwengu, nami ninataka ujenge safina. Chukua mbao shambani mwako, wala—wala usifanye miti ya vivuli tena, lakini nataka ujenge safina, upate kuyaokoa maisha yako." Naye Nuhu, kwa kutii hilo, halikuendana na mawazo yao ya kisasa ya kisayansi. Mnajua, tunafundishwa, kwamba tulikuwa na ustaarabu mkuu wakati huo kuliko tulio nao sasa, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu," ustaarabu wa kisasa.

33 Na tunaambiwa na Mwanzo ya kwamba haikupata kunyesha mvua kutoka mbinguni, Mungu aliipa maji kwa umwagiliaji, dunia ilisimama wima, haikuegemea nyuma, wala hatukuwa na mvua; na huyu hapa mtu anakuja, akitokea juu ya msingi wa hati ya mkataba, aliyopewa na Mungu, kwamba hukumu inakuja, na njia pekee ya kuikwepa, kwamba kulikuwa kunakuja janga kama vile mvua, maji yangebubujika kutoka angani. Labda baadhi ya wanasayansi wao wa kisasa wangeweza kuweka vyombo vyao, na kusema, "Tunaweza kuona hadi mwezini kwa rada, wala hakuna kitu kama maji angani. Mtu huyo ana wazimu kabisa, mwacheni, atajiletea mwenyewe fedheha."

34 Kama hiyo si picha ya mwaminio wa siku hizi, leo hii, anachukuliwa kuwa mwendawazimu kabisa, ana mihemuko, ana kichaa. Namshukuru ndugu mwishoni hapa, kwa wasifu wake, "Nilikuwa mpumbavu vya kutosha kuliamini Neno." Hiyo ni sawa. Na—nataka kubaki mpumbavu. Niliona bango dogo siku moja, ninaambiwa kuhusu mtu mmoja huko California, alikuwa na bango kubwa mbele yake hapa, kasema, "Mimi ni mpumbavu kwa ajili ya Kristo," na mgongoni mwake, akiwa na

alama ya kuuliza, kasema, “Wewe ni mpumbavu wa nani?” Uh-huh.

35 Nuhu alikuwa mpumbavu machoni pa ulimwengu, siku hiyo, kwa ajili ya . . . ya Mungu, na kwa ajili ya Neno, lakini alikuwa na hati ya mkataba ambayo ingeleta faida, ingeleta faida katika kuyaokoa maisha yake. Kama nilivyosema hapo awali, huenda isikubaliane na harakati zote za kisayansi. Wanaweza kujaribu, leo, kusema hii ni mhemuko mtupu, kama ndugu mmoja alivyoshuhudia, naamini hapa, hakutaka mhemuko wowote, na hilo ni jema, nadhani kuna mambo mengi ya kuvuka mpaka yanayoendana nayo ambayo yanatenda kazi.

36 Nilikuwa nikisoma maisha ya Martin Luther, ama, historia, nayo ilisema halikuwa jambo la ajabu sana kwamba Luther angeweza kulipinga kanisa Katoliki, na kupita nayo, lakini ajabu kuu ilikuwa, mtu huyo aliweza kushikilia kichwa chake juu ya ulokole wote ulioufuata uamsho wake.

37 Ndivyo ilivyo siku hizi, si ninii sana . . . aja—ajabu kuona watu wakitoka katika mashirika na kadhalika, bali mtu anayeweza kudumu na Neno, na kushikilia kichwa chake juu ya ulokole wote unaojaribu kuufuata mwenendo kama huo, mihemuko, na kadhalika, inayojengea imani msingi juu yake, ambayo ni ya kimwili haswa, kama ndugu yetu wa thamani alivyotunukulia kuhusu Wayunani, mnaona, wanatoka, jambo lile lile, mwili, mwili, madhehebu, kadhalika, lakini mtu fulani, anaweza kushikilia kichwa chake juu ya hayo, na kudumu na BWANA ASEMA HIVI. Ni kweli.

38 Tunaona kwamba Nuhu . . . kwamba ukiisha kupokea hati hii ninayozungumzia asubuhi ya leo, hakikisho, hakikisho la wokovu, sikuzote unajaribiwa. Na daima kuna . . . Ufalme wa Mungu hauji kupitia, kwa kuuchunguza, nasi tunajua kwamba unajaribiwa, kila mwana amjiaye Mungu hana budi kufunzwa kama mtoto.

39 Nafikiri hiyo ndiyo shida ya maskini kundi letu la akina Elvis na Riki siku hizi, hawakuwa na mafunzo mazuri ya utotoni. Baba alizoea, alikuwa akinipeleka kwenye banda la kuni, nami nikapata elimu nzuri ya jinsi ya kujiadabisha, alikuwa na kijiti cha hikori kilichokuwa na amri zote kumi nchani mwake, hakika kiliniadibisha. Ni vibaya sana hatuna baba na mama, wengi wao zaidi leo ambao wangefanya jambo lile lile, badala ya kuendesha magari ya kasi, na kutangatanga usiku kucha, na binti zao wamejifunga katika baadhi ya . . . loo, mnajua ninachomaanisha.

40 Sasa, lakini unajaribiwa, unajaribiwa upate kuthibitishwa. Basi Nuhu, baada ya siku za mahubiri yake, aliposimama katika safina ya mlango wake, na kutoa, uh, mlango wa safina yake, hasa, na kutoa wito wa mwisho kabisa, ndipo Mungu akamwambia, “Nimemalizana nao. Ingia kwenye usalama ulioandaliwa.”

41 Nafikiri hapo ndipo tunaposimama, kuingia eneo hilo la usalama. Msongamano wa dhambi unakuwa mbaya sana, lakini Mungu hutupa eneo la usalama, kama nilivyokuwa nikizungumzia jana usiku, kupewa chanjo. Kaa mle ndani, usiende kutanga-tanga, kama yule ndugu alivyosema, unaweza kuyumba-yumba ukatoka humo, afadhali ukae imara. Sasa, usiende kutangatanga kwenye itikadi na mafundisho ya sharti, dumu katika Neno, dumu na Kristo; kumjua Yeye ni Uzima, sio kujua kanuni Zake za imani, sio kujua kitabu Chake, wala kujua lolote, bali kumjua Yeye ni Uzima.

42 Tunaona ya kwamba Nuhu, hebu tufanye uigizaji wake kidogo, muda unaenda, basi Nuhu akawaambia, "Huu ndio wito wenu wa mwisho, ninayo hati ya mkataba hapa, hakikisho kwamba itanyesha, sijali kanuni zenu za kisayansi zinasema nini, lakini afadhali muingie." Wakamcheka. Kulikuwa na wengine ambao walikaa karibu, bila shaka, na kusikiliza, huku wengine hata hawakuja kumsikiliza hata kidogo.

43 Basi Nuhu akaingia, nao mlango ukafungwa nyuma yake; Nuhu hakufunga mlango, Mungu aliufunga mlango. Na ndivyo atakavyofanya tena wakati mshiriki wa mwisho wa Mwili wa Kristo. . .Kamwe haitaufanya mwili usio wa kawaida kwako ama kwangu, afadhali tuingie wakati kuna nafasi, hautakuwa na vidole sita katika mkono mmoja, hata hautakuwa na kucha mbili kwenye kidole kimoja, utakuwa ni Mwili mkamilifu usio na ila. Wakati mshirika huyo wa mwisho ameongezwa kwenye Mwili huo, Mungu atafunga mlango kati ya hukumu na rehema, au, rehema na hukumu, ninapaswa kusema. Angalieni.

44 Kisha baada ya mlango kufungwa, naweza kumsikia Nuhu akimwambia mkewe, kana kwamba ningeweza kusikiliza, na mmojawapo wa hao, kama ndugu walivyonena habari zake, njia hiyo ya kunena kwa lugha kama waya uliowekwa chini ardhini, kumsikia akisema, "Sasa, asubuhi mawingu yatatanda, ndipo itakuwa—itanyesha, hii, ngu—ngurumo zitanguruma na radi itamulika, na mvua kubwa itakuja. Nimefanya niwezavyo, lakini niko ndani sasa, na mlango umefungwa; tunajua kitu cha kimbinguni kilitokea, kwa maana kamwe hatukuufunga mlango huo, Mtu fulani alifunga huo mlango, ilikuwa ni Mungu."

45 Nanyi mwajua, wakati huo kulikuwa na baadhi ya waaminio wakwamia mpakani waliosimama karibu, na kusikiliza, waliliamini nusu, labda kama yule mtawala kijana tajiri, lakini walisema, "Afadhali tupande juu. Tunajua alikuwa mzee mzuri, na kama kukitokea jambo kama hilo, tutakuwa tumesimama karibu, ambapo tunaweza, loo, tutaingia moja kwa moja, ataufungua mlango." Lakini kumbukeni, Nuhu hakuwa na njia ya kuufungua mlango.

46 Usikwamie mpakani na Mungu. Usiwe tu mwanamume mzuri au mwanamke mzuri, wewe jazwa na Roho Mtakatifu,

ubatizwe katika huo Mwili kwa Roho Mtakatifu. Usichukue uvumi, wala chochote juu yake, kaa hapo mpaka umekufa, na maisha yako ni mapya katika Kristo, na maisha yako yote yamebadilishwa. Kamwe usichukue mhemuko, msisimko, au ninii. . .usifanye hivyo, kaa hapo mpaka kitu fulani kweli kitokee ambacho kinakubadilisha kabisa.

47 Nuhu ndani, ndipo sasa waumini hawa wakwamia mpakani wakaja kisiri na kusema, "Huenda ikanyesha, kama yule mzee alivyosema, jambo fulani lilifanyika, jambo la kushangaza sana." Vivyo hivyo ulimwengu unaweza kuliona siku hizi, kwamba jambo fulani linatendeka.

48 Hata asubuhi ya kwanza Nuhu alipoamka akapanda juu kuchungulia dirishani, jua lilichomoza angavu tu kama lilivyowahi kuwa. Ningewazia Nuhu aliangalia juu, akasema, "Ngoja kidogo, hebu tuone kama nilikuwa sahihi." Akarudi kwenye Neno, kwenye wito wake, kwenye ahadi yake, kila kitu kilikuwa sawa kabisa. "Naam, Yeye—Yeye ameicheleweshatu, labda itakuwa kesho." Kesho yake jua likachomoza. Vema, mwaminio mkwamia mpakani, akawa mkosoaji pia, kasema, "Mnaona, ilikuwa ni bure." Akatoka nje.

49 Lakini hatimaye, baada ya Mungu kumpa jaribu lake la mwisho, kwenye siku ya saba, asubuhi hiyo, anga zilikuwa nyeusi, ngurumo zilikuwa zikinguruma, na radi ikimulika, ndipo matone makubwa ya mvua yakaanza kuanguka, na u—ulimwengu wenye hofu wa watu ukaanza kupiga mayowe na kuitafuta safina hiyo, lakini ilikuwa imechelewa kupita kiasi, kama yule mwanamwali aliyelala aliyebisha mlangoni. Ilikuwa imechelewa kupita kiasi. Usingoje hadi wakati huo, njoo sasa.

50 Angalieni, halafu, baada ya haya yote, mvua ilizidi kuwa kubwa, mitaa ikaanza kujaa, mifereji ya maji machafu ikafurika, maji yakaanza kufurika, baadhi yao wakasema, "Tutajijengea tu mashua na kuelea. Tutajitafutia gogo la mpopla." Hivyo ndivyo wengi sana wanavyofanya siku hizi, kujaribu kuelea juu ya gogo la mpopla, lakini tunaona kwamba lilizama; nao walifikiri wangeweza kujenga mashua, nayo ingekuwa sawa, lakini mashua zao zikazama.

51 Hivyo ndivyo mnavyowazia siku hizi, kwamba tunaweza kuunda dhehebu, au kuingiza watu ndani yake kwa kuwaelimisha, itasonga kwa vyovyote vile kama imejengwa na Mungu au la, bali kitu pekee kitakachoshinda jaribio ni Kanisa lililojengwa na Mungu kwa Neno, lililojazwa na Roho Mtakatifu, inabidi iwe imeagizwa na Mungu, imevuviwa na Mungu, mwanadamu hana la kufanya katika hilo, ni Mungu na Yeye pekee.

52 Maji yakaanza kupanda juu ya safina, Bibi Nuhu na pengine wakwe zake walikuwa wakishangaa, Nuhu akasema, "Tulieni kimya, Mungu alitoa ahadi, hakikisho letu limehakikishwa

kabisa kwetu." Naye alijua ya kwamba ujenzi wake ulikuwa sawasawa na maagizo yake. Nami nashangaa leo kama tungeweza kutazama, na kuangalia pande zote, na kupata kujua kama ujenzi wetu ni sawasawa na yale maagizo, kwa maana alisema, "Mtu akiniamini Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Ninashangaa kama ujenzi wetu utalingana na maagizo ambayo tumepewa.

Lakini Nuhu alikagua, kila kitu, kila kona ilitiwa lami. Akasema, "Mama, haina budi kufanya kazi, Mungu aliahidi hivi."

"Mbona," akasema, "Niliangalia nje, nami nikaona akina Jones," au kadhalika, "mashua yao ilizama chini kabisa, na yetu ingali imekaa ardhini!"

53 Inahitaji tu mateso zaidi kidogo, hukumu zaidi kidogo ya Mungu kuyaleta. Hatimaye maji yakawa yenye kilindi zaidi na zaidi, baada ya kitambo kidogo familia nzima ikahisi kitu kikisogea, ikaondoka ardhini. Ninataka tu kuwa ndani Yake, moja ya siku hizi, kwa namna fulani ninachoshwa na maskini nyumba hii ya wadudu, kwenye umri wa miaka hamsini na mitatu mimi—mimi, moja ya siku hizi, natarajia kuhisi kitu kikisogea, tunataka kuondoka. Safina ilikuwa ikielea juu, wakati zingine zilizama, safina ilikuwa ikielea juu; Mungu katika Neno Lake alikuwa ameitimiza ahadi Yake. Shetani alimjaribu, Shetani alijaribu kumvunja moyo, alijaribu kumvunja moyo kupitia watu wa siku hizo, dini za siku hizo, kupitia sayansi ya siku hizo.

54 Nilisoma gazetini, jana, naamini ndivyo, hivi majuzi, ambapo sayansi imegundua njia ambayo mwanadamu si lazima afe, ana uzima wa milele. Vema, kwani wanafikiri hilo ni jambo jipya? Tumekuwa nalo kwa miaka elfu mbili; wanadhani wamepata kitu kipya! Kama vile David duPlessis alivyosema wakati mmoja, "Urusi ilijigamba kwa sababu walikuwa na mtu angani, tumekuwa na Mmoja angani kwa muda wa miaka elfu mbili. Tuko mbele yao sana hata hawajui walipo." Hakika. Mwombezi kati yetu na Mungu, pamoja na hakikisho, "Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu," hukumu zitakapokuja. Je, hutaki kuvutiwa na hati ya mkataba kama hiyo? Unapaswa kuvutiwa, kwa sababu zingine zote zitashindwa. Hiyo ni kweli kabisa.

55 Hatimaye, wakati hiyo safina hatimaye ilifanya mkutuo wake wa mwisho na kuruka wakati ikiondoka chini ardhini, Neno lilileta faida, nayo hati ya bima ikaleta faida, ilimwokoa yeye pamoja na watu wa nyumba yake. Ninashukuru sana kwa hilo. Tungeweza kukaa kwenye hilo kwa muda mrefu, lakini tutaenda mbele kidogo.

56 Kulikuwa na mtu mwingine ambaye ningependa, mwenye hati ya bima, kumjulisha kwenu asubuhi ya leo. Hapana

shaka ila mmesikia habari zake, jina lake lilikuwa Danieli. Alichukua hati hii ya mkataba wa hakikisho la Uzima, naye akachukuliwa akapelekwa mpaka Babeli katika siku zake, lakini Danieli, kwa kuwa alikuwa mmiliki wa hiyo hati ya mkataba, aliazimu moyoni mwake kutotia najisi hati yake ya mkataba, hakuwa anaenda kutia najisi uwekezaji wake. (Sasa, nitafikia ulichosema.) Unayo hati ya mkataba, lakini usiitie najisi, kama unayo, acha kuyumbayumba na ulimwengu, jiepushe nao. Naye Danieli aliazimu moyoni mwake kwamba hatautia najisi urithi wake kwa vyakula vya mfalme.

57 Sasa, baadhi yenu ninyi wanawake acheni nywele zenu zianze kukua. Kweli. Baadhi yenu wanaume, anzeni kufanya jambo fulani. Aibu kwenu wahubiri ambao, mnaona aibu kulisema, Mungu awarehemu, unaogopa utatengwa na dhehebu lako. Vipi kuhusu kutupwa nje ya safina? Kumbuka, Ndugu, ni Neno la Mungu linalosema hivyo.

58 Usiuchafue uwekezaji wako. Ikiwa umewekeza, basi ushikilie, na uuweke mahali pa salama moyoni mwako, ndani ya nafsi yako, kaa nao, usiuchafue na mambo ya ulimwengu. Enyi kanisa, mrudieni Mungu, jiepusheni na mambo haya madogo madogo mnayoyafuatilia, wa Umoja wakiwafukuza, mnajiunga na—na Assemblies, Assemblies wakiwafukuza, mnaenda kwenye Church of God, acheni kuuchafua u—urithi wenu, acheni kuuchafua uwekezaji wenu, nilipaswa kusema, rudini, udumisheni safi, mfanyieni Mungu kazi.

59 Ninaweza kuwaita, na kuwajulisha kwamba Danieli, iliyaokoa maisha yake, walipomtupa katika tundu la simba, simba hawangeweza kumla, kulikuwa na kasoro fulani, kwa maana Malaika wa Bwana alitumwa kumlinda, na ikayaokoa maisha yake. Na ikiwa kuna kitu chochote ambacho ni kizuri kwa mwanadamu yeyote, ni uhai. Ni nini kikubwa kuliko uhai?

60 Ni upi...? Je, daktari angeweza kusimama hapa asubuhi ya leo, na kuzungumza juu ya kidonge, ambacho alikuwa amevumbua kwa sayansi, kukufanya uishi miaka mia moja, au miaka elfu moja? Mbona, unge—ungeuza kila kitu ulichokuwa nacho ukakinunue. Hakika, ungeuza, uhai ni wa thamani. Lakini ninajaribu kuwaambia kuhusu...sera, bima, ya hakikisho, kwamba huishi kwa muda wa miaka mia moja, huishi miaka elfu moja, unaishi Milele, kwa sababu ni hakikisho la Uzima wa Milele, nasi tunalitaka hilo.

61 Wale wana wa Kiebrania, pia walikuwa na hati iyo hiyo ya mkataba na hakikisho, nao bila shaka hawakuwa wanaenda kusujudia chochote kinyume na Neno la Mungu, haijalishi ni mambo mangapi walijaribu kuweka mbele yao, "Huna budi kujiunga na *hili*, la sivyo tutakutupa nje," walidumu waaminifu kwa Neno, hawakusujudia sanamu yoyote, ndipo hukumu

ilipokuja, maisha yao yaliokolewa, kwa maana walikuwa wana hati ya mkataba ninayozungumzia.

62 Simoni Petro, tunaweza kunena habari zake kwa muda kidogo, kwa sababu alitajwa asubuhi ya leo. Na yeye ndiye... mmoja wa wale mitume, na ambaye alikuwa na funguo za Ufalme, kwa maneno mengine, maarifa, jinsi ya kuifungua milango ya Ufalme, nasi tulizungumzia hilo jana usiku. Huo ufunguo uliufunga mlango, na kuufungua, nasi tulisikia juu ya hayo jana usiku, ule msingi asili. Hakuna njia ya kurudi, ni kurudi tu mahali hasa ulipoanzia. Ndugu alisema asubuhi ya leo, akinena juu ya Simoni Petro, na yale aliyofanya, angalieni mahali alipoanzia, alianza kutoka katika Matendo, hapo ndipo Kanisa lilipoanzia, na hapo ndipo Kanisa halina budi kurudi, kurudi kwenye maagizo yale yale, Neno lilo hilo la Mungu na kulifuatilia kabisa. Iwapo tumeliacha, basi tulirudie, njia pekee ya kutokea vizuri ni kurudi nyuma, upate kunyooshwa.

63 Mimi hupiga risasi, kupiga kwa ustadi, nami nimepata vikombe vingi. Na hivi majuzi, Bwana akiujua moyo wangu, akijua ninahitaji kupumzika kidogo, aliniruhusu kupiga risasi kitu cha ajabu sana, nikiwa na bunduki ya kawaida ya Winchester .22 muundo 70 kwenye uwanja wa shabaha, nilipiga risasi tisa kwenye shimo moja. Wawili wa kundi la wanaume waliosimama pale waliweka dango nyuma, kasema, "Naamini unakosa shabaha." Ilikuwa ni kitu gani? Nilikuwa nimeichokora-chokora bunduki hiyo, na kuipekua, na kadhalika, mpaka kila mtetemo mdogo ilibidi uwe sawa, na kama ilikosa shabaha, kuna kasoro mahali fulani. Kampuni ya Winchester ikasema, "Bunduki hiyo itapiga iachie inchi moja tu kwenye yadi ishirini na tano," nami nilikuwa nimepiga risasi tisa kwenye shimo moja kwenye yadi hamsini, haidhuru walisema nini, ilikuwa imefanya kazi hapo awali, itafanya kazi tena.

64 Hivyo ndivyo ninavyosema leo. Wanasema, "Wewe... Hatuwezi kuwa na Pentekoste kama waliyokuwa nayo wakati huo, watu hawataamini jambo hilo, huwezi kulifanya. Hatuna budi kuwa na kanisa, hatuna budi kuwa na dhehebu, hatuna budi kuingiza elimu ndani yake," na kadhalika. Kama ilifanya kazi huko nyuma kwa wavuvi wasio na elimu ambao wangeweza kuliamini Neno la Mungu, kama lililenga shabaha wakati huo, kama liliponya wagonjwa, kama lilifufua wafu, litafanya vivyo hivyo leo. Ikiwa mtetemo sahihi umewekwa kwenye bunduki, italenga shabaha moja kwa moja, usipofaulu, rudi ukaichunguze bunduki yako, kwa hiyo, rudi, uyachukue yale maagizo, na upate kujua mahali tulipokosea; hivyo ndivyo tu ninavyojua kulifanya. Lakini itafanya hivyo, maana ililenga hapo awali, italenga tena. Kama ilifanya kazi kwa mitume bila madhehebu, bila kanuni za imani, pasipo kuwa Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, au *lolote lile*, ilifanya kazi kwao kwenye Neno la Mungu, itafanya

kazi kwangu kwenye Neno la Mungu, itafanya kazi kwenu kwa Neno la Mungu.

65 Lakini huna budi kujua zilipo skrubu zako zilizolegea, wakati mwingine unazo, samahani, nyingi sana, baadhi yao hata hubana sana, inakubidi kuilegeza kidogo, kweli, ili ipate kutikisika. Kama vile mwanamuziki na—na gita lake, akijaribu nyuzi zake, hana budi kujua mlio wake. Mtu aliyejazwa na Roho angeweza kujua mlio wake, kama iko mbali sana na Biblia, au nyuma sana ya Biblia, haina budi kuwa moja kwa moja katika Biblia, sawasawa kabisa na BWANA ASEMA HIVI, haina budi kulengwa vizuri, ndipo itaelekezwa, kisha italenga shabaha.

66 Petro alikuwa mvuvi, alikuwa amekosa shabaha kwa muda mrefu. Baba yake alimwambia kabla hajafa, "Pengine, mwanangu, mimi ni mzee, ninamtazamia Masihi, tumemtazamia tangu Edeni, pengine hatakuja katika siku zangu, lakini anaweza, katika zako. Lakini usidanganywe, mwanangu, kuna mambo mengi yanayokuja kila wakati ambayo yanasema kuwa ni Masihi, lakini sisi, Masihi ajapo, kumbuka, inatupasa kukaa na Neno jinsi Masihi atakavyokuwa."

67 Wengi wao. . . Mnajua, kulikuweko na Yesu wengi walioinuka kabla ya Yesu Kristo. Kulikuwa na viongozi walioinuka na kuwavuta watu nyikani kwa dini potovu na vikundi vya madhehebu, lakini halikuwa jambo sahihi, waliangamia pamoja nayo, kama vile uasi wa Kora, aliyesema, "Ni nani mtakatifu? Musa anafikiri yeye ndiye changarawe pekee ufuoni, kunao watu wengine watakatifu." Lakini Mungu alikuwa na njia Yake, na Mungu alikuwa na mtu Wake, na Mungu alikuwa na mambo Yake. Mungu analo Neno Lake, na ni nani atakayelipinga, kulikanusha Hilo? Dumu Nalo. Sasa, angalieni.

Kasema, "Simoni, mwanangu, ajapo Masihi, Musa, kwa Neno, alisema ya kwamba angekuwa nabii kama yeye."

68 Andrea alipokuwa ameenda huko, akamwona Yesu, alirudi na kujaribu kumwambia, nafikiri Petro alitikisa kichwa chake, kasema, "Mimi ni mvuvi, nimewekeza kwenye nyavu za baba yangu, ninaenda kuvua samaki, hiyo ndiyo kazi yangu. Nami ni Farisayo, kwa hiyo niliiacha tu iwe hivi, ninaenda kanisani, mimi ni mzuri kama mtu mwingine yeyote. Hivyo tu. Hilo ni jema. Mimi ni mfuasi wa kanisa ambalo baba yangu alikuwa mfuasi wake, ama, mapokeo, nitaendelea tu na hayo."

69 Lakini siku moja akaenda Mbele ya Huyu, na mara alipokuja katika Uwepo Wake, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Sio kwamba tu alimjua yeye, na kwamba alikuwa nani, bali alimjua baba yake mzee mtauwa, ambaye alikuwa amemfundisha, nayo yalikuwa ni kulingana na Neno, Nabii. Petro aliwekeza, akaacha nyavu zake. Akasema, "Njoni mnifuate, nitawafanya wavuvi wa watu." Ni tofauti jinsi gani

na yule mtawala kijana tajiri aliyetaka kudumisha mali yake! Lakini aliacha kila kitu alichokuwa nacho apate kumfuata Yesu.

70 Ilikuwa ni Nathanaeli, au, Filipo, aliyeenda na kumwambia Nathanaeli, labda alikuwa na shamba kubwa la mizeituni, alikuwa huko akilikagua. Basi Filipo alipomweleza juu ya yale aliyokuwa ameona, alikuwa akikosoa kidogo mwanzoni, lakini akaja tu kuhudhuria mmojawapo wa hiyo mikutano. Na mara alipomwona...

71 Akiwa ni mso—msomi wa Maandiko, alijua jinsi Masihi angekuwa, na kama ilikuwa ni sawa kuliacha kanisa lake alimokuwa, watu hawa wa kiorthodoksi waliokuwa wakimkataa Yesu, wakiitupilia mbali hati ya mkataba, wakisema, "Haikufaa chochote; haingeweza kuaminika; alikuwa mwanadamu akijifanya mwenyewe Mungu; alikuwa Beelizebuli; alikuwa mshenzi; hakuwa na usuli; alizaliwa mwana haramu; hakuhudhuria shule zao; hakuelimishwa katika seminari zao; aliyapinga mafundisho yao; alikuwa akiyavunja makanisa yao; nayo mafundisho Yake yalikuwa yanawazuia watu." Hilo ndilo alilodaiwa kufanya, wakamwita, "Beelzebuli," na kusema, "Aliwadanganya watu kwa mafundisho Yake." Sasa, hayo ndiyo yaliyokuwa yameingizwa ndani yake.

72 Lakini mtu huyu mtauwa, Nathanaeli, mara alipoenda Mbele za Yesu, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Kasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, nilikuona."

73 Akawekeza. Hapo alisimama kuhani wake na wote, hakuona haya, alikuwa amepata kitu halisi, alikuwa amemwona Mungu akifanya kazi. Alifanya nini? Alisema...Akakimbia na kuanguka miguuni Pake, na kusema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli." Akawekeza, jina lake haliwezi kupatikana na mauti; kulikuwako na wale pale walioliicheka, sijui mahali walipo leo, hiyo ni juu ya Mungu.

74 Hebu tuone kuhusu mwanamke mmoja. Kulikuwa na mwanamke, labda mshiriki wa kanisa mahali fulani, naye akaachiliwa kuzurura, huenda alikuwa na nywele zilizokatwa na kadhalika pia, pengine alikuwa ndiye mtindo wa siku hizo, lakini siku moja alikuja kwenye kisima ambapo palikuwa na Mgeni ameketi, Myahudi, dhidi ya mandhari kidogo yenye mapazia nyuma yake. Ndipo alipokuja pale na...Alikuwa na njia yake ya kujipatia riziki, na labda alikuwa na...vipande kadhaa vya dinari ya Kirumi mfukoni mwake basi, soksi yake ndogo aliyokuwa amezibebea. Naye akaenda pale kuchota maji. Alikuwa amezurura usiku kucha, labda yapata saa tano akafika pale, sijui, lakini hebu tuseme tu ilikuwa hivyo.

75 Basi alipofika pale, alimwona Mtu, Mtu wa kawaida, sio kuhani, hakuwa na bango fulani la kimadhehebu juu Yake, bali

ni Mtu wa kawaida tu, naye akamtazama, na Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.”

Akasema, “Sasa, Wewe ukiwa Myahudi, unajua hiyo si sawa, mimi ni Msamaria.

76 Akasema, “Lakini kama ungejua ni Nani uliyekuwa ukisema naye, ungeomba. . . ” Mnaona, hakujua kwa mwonekano wa nje, Alikuwa ni Mwanadamu tu, lakini alionekana kuwa mkali sana katika yale aliyosema, “Kama ungejua ni nani unayesema naye. . . ” Napenda hilo. Kama maskini yule mwanamke katika kung’ang’ania kwake, maskini yule mwanamke wa Kiyunani aliyemjia Yesu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Kasema, Yeye akasema, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

77 Ilimshangaza. Akasema, “Naam, sina mume.” Mnaona, aliishi katika dhehebu, wanawaruhusu waolewe na chochote kile, na kuolewa tena, na. . . Mnaona? Kasema, “Sina mume.”

78 Kasema, “U—umesema ukweli. Umekuwa na watano, na unaishi na mmoja sasa, kwa hivyo yeye si wako; wako wa kwanza alikuwa ndiye mume wako halali.” Mnaona? “U—u—u—unaishi hivyo.”

79 Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.” Ni tofauti ya jinsi gani na kuhani msomi aliyesema Yeye alikuwa Beelzebuli, mpiga ramli, ama ibilisi! Kasema, “Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sasa, tunajua. . . Nimefundishwa, mimi ni Myunani, ama, Msamaria, hasa, nimefundishwa ya kwamba ajapo Masihi atafanya mambo haya, hii itakuwa ndiyo ishara Yake.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

80 Upesi sana yeye akawekeza. Aliwekeza, kisha akakimbilia mjini, na wala asingeweza kutulia, alikuwa amepata lulu ya thamani kubwa, alikuwa ameuza vingine vyote.

81 Mnajua desturi katika siku hizo, haikuwa sawa kwa mwanamke kwenda mtaani, mwanamke wa aina hiyo na kuzungumza na wanaume. Lakini ati kumzuia! Ati ujaribu kumzuia! Alikuwa amepata kitu fulani, kilikuwa ni halisi.

82 Kama Nathanaeli, haikuwa uadilifu kwa kanisa lake yeye kumfuata yule Mgalilaya, *anayejiita* nabii, ambaye walikuwa wametaja kuwa ni Beelzebuli. Haikuwa sawa kwake kufanya, haikuwa ya kikanisa, haikuwa ya kimaadili, angefukuzwa *kanisani* kwa ajili yake. Lakini ati kumzuia! Alipata kitu kilicho halisi.

83 Mwanamke huyu alipata kitu kilicho halisi. Haikuwa sawa kwake kupiga kelele hivi mtaani, alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, alikuwa ametiwa alama, lakini alikuwa amesamehewa. Alipata kitu kilicho halisi, wala usingeweza kumzuia, kama kuzima moto siku yenye upepo, alikuwa

akiwaka moto, furaha na amani ya msamaha wa dhambi. Hakutaka kisima cha Yakobo tena, alikuwa amepata Chemchemi inayobubujisha Uzima wa Milele ndani Yake. Aliacha mtungi wake pale na kusema, "Nimemalizana na kitu hiki, nataka kuwekeza katika *huo*." Alikuwa mwanamke mwenye akili jinsi gani, hakika, alipata kitu cha kuwekezea.

84 Hebu tumchukue mhusika mwingine. Nilikuwa nikitaka kuzungumza juu ya maskini yule mwanamke wa Kiyunani kwa muda kidogo. Mnaona, alikuwa na upinzani mwingi, mnaona, jambo la kwanza, huenda ilikuwa, alikuwa Myunani, hakuwa Myahudi, bila shaka watu walimwambia, wakasema, "Sasa, ngoja kidogo, kumbuka, dhehebu lako haliufadhili huo." Haikuleta tofauti yoyote kwake, alikuwa amesikia, alikuwa na haja, na unapokuwa na haja, nawe usikie ya kwamba kuna kitu fulani cha kukusaidia, hakuna kitakachokuzuia. Ikiwa Mungu anaita moyoni mwako, huwezi kulizuia, hakuna anayeweza. La, bwana, unaenda kwa vyovyote vile.

85 Ninaweza kuwazia dada wote wa kanisa walisema, "Vema, utakuwa lawama miongoni mwa watu." Hilo halikumzuia, aliendelea mbele. Kundi lingine likakutana naye, likasema, "Mume wako ni mfanyabiashara, atakuacha ukishuka kwenye kundi hilo la hao watakatifu wanaojibingirisha." Hilo halikumzuia, aliendelea kwa vyovyote vile; aling'ang'ania.

86 Ni vizuri kung'ang'ania wakati unapojua kile. . .Mtu yeyote anayeweza kufanikisha chochote atang'ang'ania. Watu katika nyakati zote wamekuwa wavumilivu, kama walifanikisha chochote. Washington, baba, alivyoitwa, wa taifa letu, kwenye Bonde la Forge aling'ang'ania, haidhuru Delaware ulikuwa umeganda jinsi gani, aliomba usiku kucha, alijua ilikuwa ni lazima avuke mto huo, naye akauvuka, haidhuru ni nini kilichotukia, aliuvuka kwa vyovyote vile; alikuwa anang'ang'ania.

87 Basi baada ya mwanamke huyu kufika kwa Yesu, angalieni hapo! Hivi ndivyo imani halisi ifanyavyo: Unapopata lulu, unapopata hati hii ya mkataba, sijali ni watu wangapi wanajaribu kukuvunja moyo, kama watakutoa kanisani mwako, kama wakifanya chochote wanachotaka, bado unang'ang'ania, unataka hiyo hati ya mkataba.

88 Hivyo ndivyo Yakobo alivyokuwa, haikuleta tofauti yoyote kile kilichombidi kufanya ili kupata hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza, aliitaka. Nasi tunafikia hali hiyo, tunakuwa na shauku kubwa, ndipo tunang'ang'ania. "Vema, ninawaambia, mimi, ah, Mama alikuwa Mpentekoste, ningeomba usiku kucha, lakini nimeninii, mnaona, nimechoka sana." Hummfu! Unahitaji Sumu kidogo, kile unachohitaji, kitu cha kukufanya ung'ang'anie.

Akaingia ndani haraka, akaanguka mbele ya Yesu, naye akasema, "Ewe Mwana wa Daudi . . . " Yeye hakuwa Mwana wa

Daudi kwake, alikuwa Myunani, Mmataifa.

89 Hakumjali, halafu hatimaye akamgeukia, Naye akasema, “Sijatumwa kwa dhehebu lako, nimetumwa tu kwa kondoo waliopotea wa Israeli, hao ndio tu niliotumwa kwao.”

Akasema, “Lakini Bwana . . . ” Hilo—hilo alilipata vizuri, sio *Mwana wa Daudi*, bali *Bwana* kwake, “Bwana . . . ”

Akasema, “Na jambo lingine, ninyi si kitu ila kundi la mbwa, wala si haki kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwapa mbwa.”

90 Loo, si Mpentekoste angelipuka kwa hilo! Um-hum. “Unafikiri nitamwacha Mbaptisti aniambie jambo hilo na apite nalo? La, bwana, huh-um, ama wa Umoja, ama wa Utatu, ama *nini*?” La, bwana. Ungesukuma pua yako hewani na kuondoka. Lakini si yeye, ilimbidi ku—kuwekeza, alikuwa na haja ya uwekezaji. Amina. Haidhuru, yeye . . .

91 Imani halisi ya kweli daima itakubali Neno la Mungu ni kweli, haijalishi hali ya mambo ikoje. Alisema, “Ni kweli, Bwana, hukutumwa kwetu. Ni kweli, Bwana, kwamba mimi si kitu ila mbwa, lakini hebu nikupe upande wangu wa jambo hilo, sitafuti baraka walizo nazo, natafuta makombo.” Loo!

92 “Sasa, Bwana, kama ukiniruhusu nijing’arishe, nishuke kule, na kuniweka shemasi kanisani, kama ukiniruhusu niwe mzee wa jimbo, kwa namna fulani nitalizingatia.” Wewe mnafiki, huelewi. Unataka kuja kuokota makombo. Unataka kuja na . . .

93 “Bwana, ikiwa utanipa bila kunena kwa lugha, au kama ungenipa bila kupaza sauti, kama ungenipa bila vitu hivi vingine, uache tu nimpokee, u—unimwagilie tu ndani yangu polepole, Bwana, kwa njia nzuri ya adabu.” Mungu halifanyi kulingana na njia yako, Yeye hulifanya kulingana na njia Yake Mwenyewe. Unaona?

94 Nikihubiri wakati fulani uliopita, ndipo mwanamke mmoja akaniambia, au, si mwanamke, ilikuwa mwa—mwalimu wa shule ya Jumapili katika Kanisa la Kwanza la Baptisti, kasema, “Billy, nisingeweza kuingia kanisani kukusikiliza, bali nilikuwa nimesimama nje.” Kasema, “Nilikuwa nikifurahia ulichokuwa ukisema lakini mwanamke huyo akasimama.” Kisha akasema, “Alianza kulia, na akakimbia huku na huku kwenye marefu ya kanisa,” akasema, “kelele hizo zote zilifanya baridi ipitie mgongoni mwangu.”

95 Nikasema, “Unajua nini? Ikiwa unafikiri hizo ni kelele, unaishi katika ulimwengu mtulivu sana uliowahi kuishi. Um-hum. Utaganda hadi kufa, endapo utawahi kufika Mbinguni, kwa maana ukienda Mbinguni, itakuwa . . . ni kupiga mayowe na kupaza sauti na kumsifu Mungu mchana na usiku, Malaika wanaokizunguka Kiti cha Enzi, wakilia, ‘Mtakatifu, mtakatifu,

mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi!' Iwapo uko kuzimu kuna kulia na kuomboleza na kusaga meno. Unaishi katika sehemu tulivu mno." Bila shaka.

96 Sasa, lakini maskini mwanamke huyo Myunani aling'ang'ania, akasema, "Naam, Bwana, ninakubali kwamba yale usemayo ni kweli, wala sitafuti, labda, kuwa kama wengine wao, lakini mimi . . . "

97 Basi kumbukeni, hakuwa ameona muujiza, hakuwa ameona lolote la mambo haya, lakini kulikuwa na imani mle ndani iliyoamini kuwa hicho ndicho kitu alichohitaji kwa bintiye. Na wakati Yesu, mwujiza wa kwanza aliofanya pale, juu ya mwanamke huyu wa Mataifa, Yeye alisema, "Imani yako ni kubwa." Mnaona, hilo lilimgusa Yeye kuona ya kwamba alikuwa na bidii sana.

98 Shida ya watu siku hizi, hatuko makini sana kuhusu mambo haya, *tunachunga* maneno yetu, tunaogopa kusema kitu ambacho si cha maadili. Mungu aliahidi kukijaza kinywa chako, jiachilie Kwake, "Usifikirie chochote utakachosema." Lakini tunaliambatanisha na maadili sana, "Nikisema neno kulingana nalo, dhehebu langu halitaliamini," watafukuzwa, mauaji ya kukusudia, naam, kuna adhabu kwake, mwajua. Um-hum.

99 Kulikuwa na mtu aitwaye Nikodemo, aliona kitu *Fulani* ndani ya Yesu ambacho kilikuwa sahihi. Alikuwa mzee, mtu mashuhuri katika dhehebu lake, nanyi mwajua, alitaka kuwekeza maana alitaka Uzima wa Milele. Naye akamjia Yesu usiku, inaonekana benki zilikuwa zimefungwa, lakini benki Yake iko wazi sikuzote, mchana au usiku, imefunguliwa sasa hivi. Alikuta benki wazi, naye Yesu akampa maagizo. Alitaka Uzima wa Milele, na hapo akawekeza katika Uzima wa Milele. Tunaona makundi haya yote, na muda unaenda, hebu tuyamalizie.

100 Tunaona katika Luka 24:49, ya kwamba Yesu aliwaambia watu hawa, ambao walikuwa wametoa kila kitu walichokuwa nacho, nao walikuwa wakijiandikisha kwa ajili ya hati hii ya mkataba ya Uzima wa Milele, Luka 24:49, anawaambia kwamba atawapa faida juu yake, alisema, "Sasa, ili mpate faida yenu, ondoeni tofauti zenu zote kutoka kwenu, acheni kubishania kama wewe ni Mworthodoksi wa Kiyunani, ama kama wewe ni Mbaptisti, Mpresbiteri," kama ndugu alivyosema asubuhi ya leo, mweusi au mweupe, manjano, kahawia, "nendeni huko katika mji wa Yerusalemu, mkangoje hata nitakapoituma." Naye alikuwa na mia moja na ishirini huko juu wa kujiandikisha. Nao wakajiandikisha, kisha wakaenda huko kupata riba yao juu ya uwekezaji wao, ndipo ghafla ikaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Riba yao ililipwa, daima huleta faida.

101 Siku ya Pentekoste, kulikuwa na watu wapatao elfu tatu ambao walitaka kupata moja ya hizo hati za mkataba, naye Petro akawaambia jinsi ilivyoandikwa, akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu. Na ndipo Mungu atawapa riba yake papo hapo, mtapata faida." Amina. Je, unavutiwa na hati ya mkataba? Vema, ni kwa ajili ya yeyote atakaye, hiyo ni kweli, yeyote atakaye.

102 Baadaye kidogo, kulikuwa na kijana tajiri jina lake Paulo, naye alikuwa akizunguka-zunguka akiwavuruga watu hawa, naye alikuwa akienda zake Dameski, alijua ya kwamba kulikuwa na Mungu, bali alifikiri hilo lilikuwa ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Kwa nini? Hakuwa amewachunguza hao wenye hiyo hati ya bima, alikuwa ameingia mbio, na alikuwa amewatesa, akawacheka. Wengi wetu tumefanya jambo lile lile tulipoliona, tuliingia ndani mbio, na kulifanyia mzaha, na kusema, "Kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Lakini siku moja, akienda zake Dameski, alibwagwa chini, naye akaangalia juu akaona ile Nguzo ya Moto iliyomwongoza baba yake, Musa, na baba zake kupitia nyikani.

Naye akasema, "Sauli, Sauli, kwa nini unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

103 Akagundua na alikuwa na hakika kwamba Mungu alikuwa amefanyika mwili na akakaa miongoni mwetu. Alijua kwa Biblia kwa sababu alielewa Neno, ya kwamba Huyo kweli alikuwa ndiye Masihi, naye alikuwa ameona thibitisho lake, na mara alipoona thibitisho lake, alikuwa tayari basi kutoa pesa, naye alikuwa anaenda kujinunulia hati ya mkataba. Akashuka kwenda Dameski, ndipo Anania akaja, akamwekea mikono, akambatiza, naye akampokea Roho Mtakatifu. Ni jambo kubwa jinsi gani! Naam.

104 Wakati alipoona hiyo Nguzo ya Moto, na kujua ya kwamba ilikuwa ni Bwana aliyekuwa amefanyika mwili...Walijua ya kwamba huyo kweli alikuwa Masihi, kwa sababu Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu, kisha nikaenda kwa Mungu." Alikuja kutoka kwenye Nguzo ya Moto, alisema katika mafundisho haya, "Musa asijakuwapo...Ibrahimu asijakuwapo, MIMI NIKO." Naye MIMI NIKO Ndiye, aliyekuwa katika kichaka kilichowaka moto, na hapa alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu, ambaye kwa kweli ni Masihi, na hapo akarudi.

105 Na kwa namna fulani ilimtatiza Paulo, nasi tunafahamu kwamba alienda katika taifa lingine na kulisomea jambo hilo kwa miaka mitatu kabla hajarudi, ndipo akaona Yeye alikuwa Neno lililofanyika mwili. Alipofanya hivyo alikuwa tayari, loo, kuwekeza maisha yake yote na kila kitu alichokuwa nacho, umaarufu wake wote, elimu yake yote, alisema, "Nilisahau kila kitu nilichowahi kujua nipate kumjua Kristo." Alikuwa tayari

kuacha mafundisho yake makuu yaliyotoka kwa Gamalieli, alikuwa tayari kurudisha makaratasi ya dhehebu lake, alikuwa tayari, maana watamfukuza kwa vyovyote vile, lakini alikuwa amegundua kitu fulani. Amina.

106 Alipata shirika la kutegemewa, kwa sababu Kristo alikuwa amekufa na kufufuka tena, naye Huyu hapa tena katika Nguzo ile ile ya Moto. Haleluya! Msiogope. Hiyo inamaanisha, "Mungu wetu asifiwe!" Alitaka kuwekeza, alikuwa mfanyabiashara mkubwa, alikuwa na akili nzuri, kwa hiyo akawekeza, na akawa mtumwa wa upendo kwa Kristo. Loo, ni uwekezaji wa jinsi gani aliofanya! Hiyo ndiyo sisi sote tunahitaji kufanya. Hiyo ni kweli kabisa.

107 Ni uamuzi wa kijinga jinsi gani, sasa katika kufunga, kwa kijana huyo mtawala, ni jambo la kijinga jinsi gani alilofanya, ni ja—jambo lisilo la kimaadili jinsi gani kwa mfanyabiashara kufanya, wakati mtu wa biashara, naye alikuwa amefanikiwa, naye alipewa nafasi ya kupokea hati ya mkataba iliyothibitishwa, Mtu ambaye alikuwa ameona ndani Yake, yeye mwenyewe, nguvu za Mwenyezi Mungu zikifanya kazi, na kujua kwamba hakuna mtu angeweza kufanya mambo hayo isipokuwa Mungu alikuwa pamoja Naye, ndipo akapewa nafasi ya kumpokea, na bila makini, akaikataa. Afadhali awe na umaarufu wa utajiri wa duniani, afadhali awe na madoido aliyokuwa akiishia. Hebu niseme hivi kwa upendo na heshima: Hilo ndilo tatizo la makanisa yetu.

108 Rabi wa Kiyahudi, wakati John Rhyn alipoponywa, mmesikia hadithi ya uponyaji wake, ombaomba mtaani, nami nikapelekwa katika sinagogi ambapo rabi mmoja alikuja kuzungumza nami, naye akasema, "Bw. Branham," John alikuwa pamoja nami, naye akasema, "uliyafungua macho ya mtu huyu kwa mamlaka gani?"

Nikasema, "Kamwe sikuyafungua macho yake."

Akasema, "Mbona, nimempa sadaka mitaani mara nyingi." Akasema . . .

Nikasema, "Anaweza kuona."

"Naam."

Nikasema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyafungua macho yake."

Akasema, "Na iwe mbali na Mungu, kuwa na Mwana, Roho kuwa na Mwana." Akasema, "Na iwe mbali na kitu kama hicho."

Nikasema, "Rabi, je, ni vigumu kwako kuyaamini Maandiko?"

"Bila shaka la, mimi ni mwalimu wake."

"Unawaamini manabii?"

Akasema, "Ninaamini."

"Katika Isaya 9:6, nabii alikuwa akizungumza juu ya Nani?"

Kasema, "Masihi."

Nikasema, "Masihi atakuwa . . . Masihi atakuwa na uhusiano gani na Mungu?"

Akasema, "Masihi atakuwa Mungu."

Nikasema, "Sasa, uko kwenye mstari."

Akasema, "Ninyi Mataifa hamwezi kumkata Mungu vipande vitatu, na kutupatia sisi."

109 Nikasema, "Huyo ni Mkatoliki, huyo sio mimi. Um-hum, um-hum. Kuna Mungu mmoja katika ofisi tatu: Ubaba, Uwana, na Roho Mtakatifu," sio Miungu watatu, hilo linamfanya kafiri, nawe usingeweza kumshindilia Myahudi hilo, wala mimi.

110 Kumbukeni, Neno ndilo linalolifanya kuwa kweli. Hilo lilitatuliwa kwenye Baraza la Nikea, naamini, wakachukua upande huo mwingine. Manabii wa kale wakarudi makwao wakiwa na ile Kweli. Uh-huh. Kamwe hutaiangamiza, inaendelea. Um-hum. Hiyo ni kweli. Naona watu wakikuna vichwa vyao na kushangaa, njoni tu kwa Mungu. Mtu akipungukiwa na hekima, na amwombe Mungu, Mungu hufunua mambo yote na kufanya Maandiko yashikamane. Angalieni.

Sasa, wakati rabi huyu, alisema, "Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana."

Nami nikasema, "Vema."

Kisha akasema, "Itakuwa . . . "

Nikasema, "Nionyeshe mahali pamoja ambapo alishindwa kuthibitisha Yeye hakuwa Mungu."

Akasema, "Mungu asingekuwa mwizi."

Nikasema, "Yeye—Yeye hakuwa mwizi."

Akasema, "Alienda siku ya sabato mashambani, na kuvunja masuke."

111 Nami nikasema, "Torati yenu wenyewe ya Walawi inawaambia kwamba mtu anaweza kupitia shambani na kula atakacho, lakini hawezi kuondoka na chochote katika gunia." Torati yake mwenyewe, aliijua, naye akageuka na kunitazama, nami nikasema, "John anaweza kuona, sivyo?"

Akasema, "Naam." Kasema, "Bw. Branham, nitakubali Yeye alikuwa Mtu mwema."

Nikasema, "Utakubali, Rabi?"

112 Akasema, "Naam, bwana," kasema, "zaidi ya hayo, nitakubali Yeye alikuwa Nabii, na kama makuhani wa hekalu wangemsikiliza Yeye, tungekuwa bora zaidi leo hii."

Nikasema, "Rabi, unaamini Yeye alikuwa Mwana wa Mungu."

Akasema, "La, la, la, la."

113 Nikasema, "Ngoja kidogo, ulisema Yeye alikuwa ni mtu mwema, ungeweza kumwamini, kama Yeye ni Nabii, hatasema uwongo, Naye alisema Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Sasa, vipi kuhusu hilo?" Naam!

Akasema, "Nikihubiri hayo," tulikuwa tumesimama kwenye Bandari ya Benton, akasema, "unaona huko chini? Ningekuwa mtaani, nikiomba riziki yangu."

114 Nikasema, "Huyo hapo Myahudi kwako." Kweli? Nikasema, "Afadhali nilale njaa, na kunywa maji ya tawi, na kula biskuti kavu ya magadi, na kuhubiri Ukweli wa Mungu, kuliko jina langu kubandikwa, kama lenu, juu ya jengo hili kwa herufi za dhahabu, na kula kuku aliyekaangwa mara tatu kwa siku." Naam, bwana, ile kweli.

Machozi yakatiririka mashavuni mwake, kasema, "Nitakuona baadaye."

Nikasema, "Sivyo. . .Hebu tumwone Yeye sasa. Mimi. . ." Lakini akarudi.

115 Basi, alipoingia mlangoni, akageuka, akanitazama, kasema, "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Aliliamini. Ati nini? Aliogopa, kama kijana huyu mtawala tajiri, kuwekeza. Um-hum. Hiyo ni kweli. Sio marabi tu, bali wahudumu, walei, wanaogopa kufanya uwekezaji huo.

116 Ni jambo la kijinga jinsi gani alilofanya mtu huyu, kufanya uamuzi kama huo. Makanisa siku hizi, umaarufu huu, huwezi kuwa maarufu na kuwa pamoja na Kristo, ukimpenda Mungu, unachukiwa na ulimwengu. Hiyo ni kweli kabisa. Maarufu, naam, bwana, sifa za mwanadamu badala ya sifa za Mungu, wanahitaji Sumu kidogo.

117 Lakini huyu kijana tajiri, sasa hapa kuna jambo kwa ajili yenu wafanyabiashara, nami sina budi kufunga, angalieni sasa, kwa hiyo mta—mtaacha hili lizame ndani ya mioyo yenu, kwa kumkataa Yesu, halikuzuia ongezeko la mali yake, aliendelea mbele, hebu tumfuate kwa muda kidogo katika Biblia, mtiririko wake wa bidhaa ukapanuka zaidi. Na ati kwa sababu biashara yako inaimarika kidogo, kamwe usiwazie kuwa, wakati wote, hizo ni baraka za Mungu, waovu hufanikiwa, mnajua. Mtu huyu, alizidi kufanikiwa, naye akafikia mahali ambapo alitajirika sana hata maghala yake yote nusura yapasuke, ilimbidi kujenga mengine mapya.

118 Sasa, aliwazia alikuwa amefanya jambo lililo sahihi kwa kumkataa Yesu na kutowekeza katika Yeye. Alidhani alikuwa. . .alikuwa amefanya lililo sahihi, kwa sababu katika mali ya ulimwengu, nitasema jambo fulani sasa, katika mali

za ulimwengu aliwazia alikuwa amefanya jambo zuri kwa sababu alikuwa amefanikiwa. Na hivyo ndivyo madhehebu yetu yanavyowazia, kwa sababu wanajiundia madhehebu, na vikundi vyao vinakuwa mamilionea na mabilionea, wanajisikia kuwa *wamewasili*.

119 Je, Biblia haikusema, "Wewe ni tajiri na umejitajirisha," kwa wakati huu, "nawe hujui ya kuwa u uchi, mnyonge, maskini, mwenye mashaka, kipofu, nawe hujui"? Ni hali ya kusikitisha jinsi gani! Wanaume na ndugu, msiwekeze katika kitu kama hicho, hakina budi kuangamia. Kwa nini usiwekeze katika kitu ambacho kimethibitishwa kote katika Biblia? Nawe wajua, pamoja na—na maandishi niliyoandika hapa, tungeweza kuwa hapa usiku wa leo, bado, kwenye maandiko haya tukithibitisha kupitia Biblia wale waliofanya hivyo na wale waliokataa.

120 Ninawaonyesha uwekezaji halisi wa kufanya: Weka maisha yako, wakati wako, pesa zako, talanta yako, weka kila kitu ulicho nacho katika Kristo. Mungu alituhakikishia hili, kwa kumfufua tena, tutafufuka katika siku ya mwisho, Yeye aliahidi hilo. Ungeweza kutazamia nini cha zaidi? Niambie uwekezaji wowote ungeliweza kufanya, ungeweza kuleta faida kama huo. Niambie unachoweza kuwekeza ndani yake, asubuhi ya leo, na kutengeneza dola milioni kumi, na kesho uwe maiti. Ingekufaidi nini? Atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote na kupata hasara ya nafsi yake? Vipi kama wewe ni maarufu, na unaitwa *Nanii*, na Shemasi, Mzee wa Jimbo, na Daktari, Askofu, Mzee, Papa, au vyovyote unavyoweza kuitwa? Hizo ni sifa za wanadamu.

121 Afadhali niitwe mtakatifu anayejibingirisha na watu, na kuwa na. . .kuwa mwana wa Mungu moyoni mwangu, pamoja na kuzaliwa upya huku Roho wa Kristo akikaa ndani yangu, Naye akilithibitisha hilo kwa kuthibitishwa kwa Neno Lake na kunifanya niishi. "Maisha ambayo niliishi wakati mmoja, siyaishi tena," Paulo alisema, hata hivyo alikuwa mwalimu na mwanachuoni, lakini alibadilisha maisha yake, alipokutana na Kristo, na kufanya uwekezaji wake katika Kristo, alikuwa mtu tofauti tangu wakati huo na kuendelea.

122 Loo, kujitajirisha, hakika mtu huyu alijitajirisha. Nanyi mnajua nini? Yesu alimwambia, kama mkiangalia hapa, Yeye alisema, "Nenda, ukauze ulicho nacho, ukawape maskini, kisha uje unifuate, uchukue msalaba wako unifuate, nawe utakuwa na utajiri Mbinguni." Unaona? Ni uwekezaji wa jinsi gani kufanya, lakini alichagua kutofanya hivyo! Sasa, vivyo hivyo Wakati wa Kanisa la Laodikia umechagua jambo lile lile, kutolifanya. Basi kumbukeni, alipotajirika sana, kama vile kanisa lilivyo siku hizi, maskini alilala langoni pake, na akapata tu makombo ambayo aliyafagia yawaendee mbwa, Lazaro, maskini wa roho.

123 Yesu alisema katika Mathayo 5, "Heri walio maskini wa

roho maana Ufalme wa Mbinguni ni wao." Hatutaki kuchukua mahali hapo, mahali hapo panapoparuza, mahali hapo pa mbali sana pa kuwa maskini wa roho, hatutaki hilo, tunataka mtu fulani atusifu, na tuwe mtu fulani mkubwa. Kama vile ndugu fulani alivyosema muda mfupi uliopita, hakika alilitia muhuri vizuri, aliposema, "Mnawezaje kuwa na imani, wakati mnaheshimiana nyinyi kwa nyinyi, au mnatamani si—sifa mmoja kwa mwingine?" Usijali mtu yeyote anasema nini, unataka sifa za Mungu, heshima za Mungu ziwe juu yako, Yeye atakuheshimu tu unapolishika Neno Lake. Vema.

124 Sasa, nasi tunaona ya kwamba mtu huyo maskini wa roho alilala langoni pake na kupigania yale makombo. Loo, labda, kama angalikuwa Jeshi la Wokovu, angalimpa senti moja alipopita, ama chochote kile, kulifanya lionekane baya sana, mnaona, lakini nafikiri aliwekeza sana katika kanisa lake mwenyewe, na dhehebu lake ambalo lilimfanya kuwa mkubwa, mtu *fulani* mkuu.

125 Lakini malipo hatimaye yakaja, hatimaye yakafika, akawa na ibada kuu ya mazishi, ninawazia maskini kapera mmoja alikuja akiwa amevaa joho pana na kusema, "Ndugu yetu mpendwa, sasa yuko Mbinguni. Loo, alifanya *hivi-na-hivi*, yeye ni mfuasi wa kusanyiko letu, sasa yuko Mbinguni. Loo, jinsi tunavyoshukuru kwa ajili ya ndugu yetu mpendwa." Jinsi ilivyokuwa tofauti na Neno la Mungu. Yesu alisema malipo yake, alikuwa kuzimuni. Alifanya uwekezaji mbaya. Na katika kuzimu akaangalia juu na kumwona yule maskini wa roho, ambaye alikuwa amefanya uwekezaji wake akiufurahia kwenye vifua vya Ibrahimu, naam, halafu basi yeye akawa ombaomba, akitamani kwamba. . . Yeye alijidai kuwa mwaminio, "Baba Ibrahimu, mtume ombaomba huyo hapa chini." Ikageuka tena, uwekezaji wake ulikuwa katika kitu kibaya, mali ya ulimwengu na sifa za wanadamu.

126 Lakini ombaomba huyu alilala pale akiumwa na njaa, naye akawa katika vifua vya Ibrahimu. "Mtume Lazaro, yuko huko, ambako anaweza kupata maji ya kunywa wakati wowote atakapo, anaweza, huko kufurahia baraka za Mungu. Mtume huku chini na matone machache ya maji vidoleni mwake, apate kugusa midomo yangu inayokauka hapa, kwa sababu miale hii inanitesa." Hayo ndiyo malipo. Ya nini? Kukataa kufanya uwekezaji sahihi.

127 Msifanye hivyo, enyi wanaume, msifanye hivyo, enyi wafanyabiashara, ni—nina imani zaidi nanyi kuliko hiyo. Ikiwa wewe ni mfanyabiashara, uza kila lulu uliyo nayo ukanunue ile Moja ya thamani kubwa, fanya uwekezaji wako katika Kristo, katika Uzima Wake ndani yako.

128 Sasa, tunatambua kwamba kila kilicho na mwanzo kina mwisho, na kuna kitu kimoja tu ambacho kamwe hakikuwa

na mwanzo, nacho kilikuwa ni Mungu. Na wakati Biblia inapozungumza pale, sidhani kama ninainukuu vibaya, mbele ya mwanachuoni wa Kiyunani, na Myunani, neno *Zoe* linamaanisha "Uzima wa Mungu Mwenyewe," basi iwapo tuna Uzima wa Milele, neno la Kiyunani *Zoe* linamaanisha kwamba tuna sehemu ya Uhai wa Mungu Mwenyewe, kwa sababu tunakuwa sehemu Yake, sisi ni mwana na binti Yake, basi tuna Uzima wa Milele, na Huo haufi, una Uzima wa Milele.

129 Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo ni Mungu. Mungu ni wa Milele, kamwe hakuwa na mwanzo, kamwe hawezi kuwa na mwisho, na njia pekee tunayoweza kuwa wa Milele pamoja Naye ni kufanyika sehemu Yake. Njia pekee niliyofanyika Branham ilikuwa ni kwa sababu nilifanyika sehemu ya Branham; njia pekee niliyofanyika wa jamii ya binadamu ni kuwa mmoja wao. Na njia pekee ninayoweza kuwa mwana wa Mungu ni kufanyika sehemu ya Mungu, ndipo sina budi kuzaliwa kwa Roho Wake. Amina. Ndivyo hivyo. Uza kanuni zako zote za imani za kimadhehebu na uwekeze katika Uzima wa Milele.

130 Wafanyabiashara, wanawake wafanyabiashara, mnaona kupitia Maandiko, wengine wengi wamekuwa wakipitia akilini mwenu, kama mjuavyo nina njia ya kujua hilo, juu ya mambo mengine, uza kanuni zako zote za imani, na madhehebu yako yote, uje upate Uzima, umealikwa, asubuhi ya leo, uje. Usikatae kama alivyofanya, alikuwa mfanyabiashara mpumbavu sana, kwa hivyo usiwe kama yeye; kuwa kama Paulo, uza umaarufu wako wote. Yeye alisema, "Sikuja kwenu kwa maneno makubwa ya elimu yangu, kwa kuwa, maana kama ningefanya hivyo, basi mngetegemea," uwezo wake, elimu yake, "lakini nilikuja kwenu katika uwezo na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, ili imani yenu ipate kutulia katika Kristo."

131 Naomba nirudie maneno yake, ama, sio kurudia, bali kulisema hivi: Sikuja nikiwakilisha dhehebu fulani. Sikuja kama mwanachuoni, maneno yangu yamekatikakatika, wengi wenu nyinyi watu wema mlio na elimu huenda hata msielewe, ni mabovu sana, bali ninakuja kwenu katika nguvu za Roho, katika madhihirisho ya Roho Mtakatifu, ambapo Mungu analithibitisha Neno Lake, ili imani yenu isitegemee kile anachofanya mwanadamu, bali kile ambacho Mungu ameahidi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

132 Kwa uchaji, Bwana, tunasimama kwenye kilele ambapo uamuzi hauna budi kufanywa, wakati huu mzuri sana wa—wa yubile ambao tunasherehekea, kwenye Maskani ya Uzima, ya mwaliko Wako, miaka hamsini iliyopita, kwa watu Wako. Nasi tumeipitia kikamilifu tujuavyo sisi. . .njia yangu ya—ya kujua, na kumtegemea Mungu, Yeye ajuaye moyo wa mwanadamu, ya kwamba ataifunua kwa njia ifaayo inayokusudiwa, ili watu

wapate kuona kule kurudia, na njia pekee ya kufanya hivyo ni kuufikia ukweli wa Neno.

133 Ninakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, kwamba hakuna hata mmoja wetu atakayekuwa mjinga kiasi cha kukataa uwekezaji kama huo. Jalia tuwekeze wakati wetu, talanta yetu, na yote tuliyo nayo, kwa sifa za Mungu, tukijua hili, kwamba haidhuru kama. . .tuliupata ulimwengu wote, tukapoteza nafsi yetu; itatufaa nini? Sifa za mwanadamu zina faida gani wakati moto wa atomiki unaiteketeza dunia? Itafaa nini leo, labda wakati makaburi yetu yataelea kwenye mchanga fulani, wakati upepo mkali uvumao. . .wakati ulimwengu huu utakaporushwa ndani ya jua huko ng'ambo, ukatupwa kutoka mahali pake, kama vile katika maangamizi yaliyotangulia ile gharika, na kutupwa, badala ya kutupwa kutoka kwenye jua, utupwe ndani ya jua? Si maji tena, lakini moto wakati huu. Nao mchanga uvume kote duniani kabla ya ule Utawala wa Miaka Elfu, nayo mawe ya makaburi yetu yatokee, "Dk. *Nanii*, Ndugu *Nanii*, ama Askofu *Nanii*," hiyo itatufaa nini wakati nafsi zetu ziko kule mahali fulani katika Umilele? Na haina budi kuwa, walio hai wanajua hawana budi kufa.

134 Kama wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, asubuhi ya leo, Bwana, sote tunatambua kuwa ha—hatuko hapa tupate kuonekana wala kusikilizwa na wanadamu, tuko hapa katika yale maumivu makuu ya Kalvari, tuko hapa pamoja na Roho Mtakatifu mioyoni mwetu akilia, kama alivyofanya kwa Bwana wetu juu ya kukataliwa Kwake huko Yerusalemu, nazo roho zetu asubuhi ya leo zinaulilia ulimwengu uliopotea. Utupe hekima tujue jinsi ya kuwakaribia, Bwana, hatutaki wapotee, Roho yeye yule ndani yetu angetuhukumu tukitaka wapotee. Lakini naomba Roho Mtakatifu alie daima, aenee kote, mpaka tuweke juhudi zote kwa talanta yetu, pamoja na wakati wetu, pamoja na pesa zetu, pamoja na kila kitu tulicho nacho, haidhuru ni kidogo jinsi gani, tunakutolea Wewe. Tusaidie, Bwana, kupeleka Ujumbe huu mkuu kwenye ulimwengu unaokufa.

135 Nina kidogo sana, Bwana, ninachoweza kutoa, hakuna uwezo, hakuna utu, hakuna chochote, lakini nina roho yangu tu, Bwana, sauti yangu, na yote ni Yako, nami nina hakika hilo linazungumza kwa ajili ya wasikilizaji hawa wote, litumie, Bwana. Kama ningalikuwa na pesa, zingekuwa ni Zako, wakati nilio nao ni Wako, kila kitu, yote kwa yote kwangu. Nisaidie, Bwana, na utusaidie sote, tunataka kuwekeza asubuhi ya leo katika Ufalme wa Mungu.

136 Tusamehe uzembe wetu. Jinsi tumekuwa wabaya sana kutafuta hazina hii kuu. . .Na jinsi Roho Mtakatifu ndani yetu anavyopaswa kuwa na shauku ile ile aliyokuwa nayo alipokuwa ndani ya Kristo, daima kufanya mapenzi ya Baba na maagizo Yake, Naye alikuja kuwaokoa waliopotea. Utupe

hiyo shauku, Bwana. Jalia usiondoke, kifuani mwetu, moto huo, kama mtumishi Wako mkuu, John Wesley, alivyosema. Usiondoke kamwe, jalia uenee zaidi na zaidi, mpaka ututupe magotini mwetu kuomba na kushawishi; jalia ututupe magotini kwenda kwenye njia kuu, na barabara ndogo, na pembeni, na katika biashara, na kila mahali, kuingia makanisani, na popote tuwezapo kufika, na kuutambulisha Uzima huu wa Milele kwa wanaume na wanawake leo hii, na yote yatakapoisha, jalia tukusanyike Nyumbani Mwako.

137 Tunapoketi hapa, asubuhi ya leo, tukitazama upande wa pili wa meza hii, nami nimemwona Ndugu Hierholzer, yule mtakatifu mzee mtauwa, nikasikia habari zake akiendesha jembe hilo, na kujiwazia mwenyewe kama mvulana mdogo asiye na viatu na, jozi ya kamba mabegani mwangu, nyuma ya jembe la kale. Huyu mtakatifu Wako mkuu, kutoka California, alikuwa kwenye ule Mtaa wa Azusa, akiwaona hao watu huku mabega yao yameinama kutokana na kazi ngumu shambani, nami nikaketi kwenye kifungua kinywa hiki pamoja nao, ni afadhali niwe hapa kuliko kuwa pamoja na Rais, nikiketi katika kundi hili la watauwa.

138 Macho yetu, wakati sisi vijana tunapotazama na kuona baba na mama zetu, jinsi walivyopiga vita wapate kushinda tuzo na kuabiri bahari zilizojaa damu, tusaidie, Bwana, kuendelea kutoka pale wanapoachia. Tujalie, Bwana.

139 Na siku moja wakati maisha yamekwisha, nasi labda tusiketi tena kwenye kiamsha kinywa kama hiki, lakini tutaketi kwenye Karamu ambayo itaandaliwa angani siku moja. Ndipo basi Mfalme katika utukufu Wake wote, huku amevaa mavazi Yake makuu asonge mbele, nasi tunyoshe mikono mezani na kupeana mikono sisi kwa sisi, “Nina furaha sana kukuona, Ndugu!” Machozi ya furaha yatatiririka mashavuni mwetu, lakini Mfalme atasema, “Vita vimekwisha, mlifanya vizuri mlivyoweza.” Ndipo kwa mikono Yake atayafuta machozi yote kutoka machoni mwetu, na kusema, “Ingieni katika furaha za Bwana, ambayo imetayarishwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu,” wakati majina yetu yalipowekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

Bwana, tusaidie tuwe na shukrani Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo, na tukutumikie Wewe. Amina.

140 Huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja, ni wangapi, asubuhi ya leo, katika Uwepo wa Utu Wake mtukufu, katika wakati huu wa kicho wa uchunguzi wa Roho Mtakatifu mioyoni mwetu, kama bado kwa kweli hujapokea Uzima wa Milele, wataniacha mimi na Bwana tuone mkono wako ukiinuliwa? huku wengine wakiwa wameinamisha vichwa vyao. Utafanya hivyo? Inua mkono wako, useme . . . Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, kote humu jengoni. Inua mkono wako,

useme. . . Mungu akubariki. Mungu akubariki. “Nataka Uzima wa Milele.” Mungu awabariki, vijana kwa wazee. Hiyo ni sawa. “Nataka kuwekeza yote niliyo nayo, nataka kuwekeza nafsi yangu, nataka kuwekeza wakati wangu, nataka kuwekeza kila nilicho nacho nipate kuurithi Uzima wa Milele. Ninahisi Kristo ananiita kufanya hivyo, nami nitafanya hivyo leo.” Mungu akubariki. Na Mungu akubariki. Mungu akubariki, naam. Kimya kimya. Mungu akubariki, ndugu yangu. Ubarikiwe, dada yangu. Hiyo ni kweli. “Nataka kuwekeza asubuhi ya leo, Mungu. Siinui mkono wangu ili mhudumu apate kuniona, ninainua mkono wangu ili uweze kuniona, Wewe unaujua moyo wangu. Nataka kulifanya, nataka kuuza kila kitu nilicho nacho, ninataka kuuza umaarufu wangu wote, mali yangu yote ya mawazo ya mambo ya ulimwenguni.”

141 Sasa, simaanishi utoe mali yako, simaanishi hivyo. Ninamaanisha, mambo ambayo unashikilia ambayo yanakuweka mbali na uwekezaji huu. Wafanyabiashara, simaanishi muachane na biashara zenu, Mungu alikuweka katika hiyo, kaa nayo, lakini weka mapato yako kwa kazi Yake kwa njia fulani. “Nitafanya uwekezaji wangu, Ndugu Branham.”

142 Je, kunaweza kukawa na mwingine? Kumekuwa na dazani moja ama zaidi. Je, kunaweza kukawa na mwingine? Mungu akubariki, bwana. Mwingine kabla hatujaomba? Mungu akubariki, ewe msichana, huo ni uamuzi mkuu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu yangu, hapo.

143 Je, kunaweza kukawa na wahudumu hapa? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. “Niko tayari, Ndugu Branham, sijali, nitadumu na Neno la Mungu, haidhuru. Sitaninii. . . Najua halipendwi, lakini nitadumu nalo, kwa hiyo Mungu nisaidie, nitawekeza asubuhi ya leo. Nitakuwa mfanyabiashara wa Mungu, nitaweka talanta niliyo nayo kwa utukufu Wake, na kwa Ufalme Wake, na kuacha kuiuzia utajiri wa dunia.” Mungu akubariki, ndugu yangu Mkristo. Mungu akubariki, ndugu yangu mhudumu. Mungu akubariki, ndugu yangu mhudumu. Hilo ni zuri. “Nitalifanya.” Mungu akubariki, ndugu yangu mhudumu. “Nitalifanya.”

144 Mungu akubariki, dada yangu. Mungu akubariki, dada yangu. “Nitauza kila kitu, nitakaa na Neno.” Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada yangu huko nyuma. Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu akubariki, dada yangu, ndivyo hivyo, Yeye anauona huo. Mungu awabariki, ndugu zangu, nyote wawili hapo pamoja. Mungu awabariki hapa, ninyi huko nje. Mungu akubariki, ndugu yangu, wewe, Dada. Hiyo ni sawa. Wewe, ndugu yangu.

145 Kumbuka, unapokuwa katika maombi, unaasi kila kanuni

ya sayansi unapoinua mikono yako. Unasema, “Ndugu Branham, hilo halifai kitu,” linafaa ukilimaanisha, inategemea unachomaanisha. Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele,” si kujifanya kuamini, lakini kuliamini kweli, na ulimaanishe. Sayansi inasema, kulingana na sayansi, nguvu za uvutano za dunia huishikilia mikono yako chini, bali una roho ndani yako iliyotoa uamuzi, kwa sababu kulikuwa na Roho mwingine ndani yako, Roho wa Mungu, alisema, “Inua mikono yako,” nawe ukaasi kanuni za sayansi, ndipo mikono yako ikainuliwa kwa Muumba wako. Kama ulilimaanisha, Yeye aliweka jina lako kwenye uwekezaji huo asubuhi ya leo.

146 Sasa, Baba wa Mbinguni, hao ni Wako, wao ni nyara za Ujumbe, nyara za Neno, nyara za Yesu Kristo, Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuwapokonya mkononi mwa Baba Yangu. Alinipa Mimi.” Hakuna mtu aliye mkuu vya kutosha kufanya hivyo. Uwalinde, Baba, uwapeleke kama vijinga vilivyonyakuliwa kutoka motoni, uwafanye kuwa mianga inayowaka kwa ajili ya Ufalme Wako. Ninawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

62-1124B Uwekezaji
Washington Youree Hotel
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org